**Maandiko yanawapa mamlaka wazee wa kanisa?**

Kwanza, maandiko yako wazi kwamba wazee wa kanisa wana kiwango fulani cha madaraka juu ya kusanyiko wanalotumikia. Katika 1 Wathess. 5:12, Paulo aliandika, “Lakini, ndugu, tunataka mwatambue wale wanaojitaabisha kwa ajili yenu, na kuwasimamia ninyi katika Bwana na kuwaonyeni.” Katika 1 Timotheo 5:12, Paulo aliandika, “Wazee watawalao vema na wahesabiwe kustahili heshima maradufu; “ Na tusisahau Waebrania 13:17, ambapo maneno ya Roho Mtakatifu yanasema, “Watiini wenye kuwaongoza, na kunyenyekea;” Neno watiini, linamaanisha “kushawishi” au “kubembeleza” na “kutumaini” na neno “wanaowaongoza” huonyesha “uwezo wa kiusimamizi.”

Pili, kuna aina mbili za mamlaka zinazoratibu kanisa. Kuna mamlaka ya kisheria, Kristo ana mamlaka yote, Mathayo 28:18-20; Efeso 1:22. Wazee wa kanisa hawana mamlaka ya kuigeuza, kuiboresha, kuongezea andiko katika mamlaka ya kisheria. Walakini linapokuja suala la taratibu, wazee wanaweza kutekeleza mambo kwa mujibu wa madaraka yao; nasi kama kundi ni lazima tuwatii. Taratibu, ni yale mambo yanayotusaidia katika kuitii amri ya moja kwa moja kutoka kwa Mungu, 1 Wakorintho 10:23; Mathayo 5:29-30; Yohana 16:7.

Tatu, pamoja na kusemwa haya yote, linapokuja suala la taratibu, Wazee siyo “mabosi,” au kujisikia kama “madikteta” juu ya kundi, 1 Petro 5:3; 3 Yahana 1:9-10. Badala yake, wanatakiwa wafanye hivyo kwa hiari, kwa busara, bila ubinafsi na kwa kunyenyekea. Watakuwa watu ambao wanathamini ushauri mzuri na wa maana kutoka kwa waumini, na kamwe hawataupuuza ushauri kwa sababu ya taratibu. Bado, mwishowe, wazee watawalao katika mambo haya watasimama mbele ya kiti cha enzi cha Mungu ili kutoa hesabu. Nasi, watakatifu, mmoja mmoja hali kadharika tutasimama mbele za Mungu kwa tabia na matendo tuliyowatendea wazee wa kanisa. “Watiini wenye kuwaongoza, na kuwanyenyekea,” Waebrania 13:17